

# MAMLAKA

## YA KIONGOZI

# UTANGULIZI.

Ndugu msomaji wangu, napenda kukujulisha kuwa, kitabu hiki cha **Mamlaka ya Kiongozi**, ni kitabu kinacholenga kuhuisha au kufufua uhai wa kiongozi, kwa maana kiongozi pasipo **mamlaka** ni kama mtu au kitu kilicho kufa. Au naweza kusema, kiongozi pasipo **mamlaka** ni sawa na gari isiyokuwa na injini. Na kwa msemu mwingine iwapo kiongozi asipokuwa na **mamlaka**, anakuwa kama kituko fulani, kwa maana nisawa na trafiki ambaye amesimama barabarani bila ya kuvaa sare, hivyo huonekana kama mpita njia.

### **MKAZO HALISI WA KITABU**

Mkazo wa kitabu hiki, ni kumjenga kiongozi yoyote kwenye maisha ya mamlaka ya kiongozi. Kiongozi anatakiwa kuishi ndani ya mamlaka au mamlaka iwe ndio sehemu ya maisha yake, aidha ajue kuwa ili uongozi wake uonekane ni lazima ionekane mamlaka ya kiongozi ndani yake, kwa kila anachokisema na kufanya kionyeshe mamlaka ndani yake.

### **HAKUNA MTU ANAYEMTII MTU BALI WATU HUTII MAMLAKA.**

Sisi binadamu wote ni sawa kabisa, lakini tunatofautiana kwa vipawa ambavyo Mungu ametujaalia, wewe ni kama mtu mwingine yoyote, na usidhani watu wanatii sura yako au umbile lako, la hasha! Bali wanaweza kukutii kwa sababu ya kuonekana kitu cha tofauti

ndani ya maisha yako, nacho ni **mamlaka ya kiongozi**. Watu wanapoiona mamlaka ya kiongozi ikitendakazi, ndipo utanza kuona watu wakinyenyekea kwako. Sio wanakutii wewe bali wanaitii ile mamlaka inayoonekana kutendakazi.

## **MANENO YENYE NGUVU YA PAULO KWA KIONGOZI**

*Maneno yanayofuata hapo mbele yana ujumbe mzito kwa kiongozi, ambayo Paulo anazungumza na kiongozi kama mimi na wewe*

2 Timoseo 2:15 *Jitahidi **kujionyesha** kuwa **umekubaliwa** na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya **kutahayari**, ukitumia kwa halali neno la kweli.*

Maneno hayo ukiyasoma kijuu juu utadhani kama ni maneno mepesi, lakini kiukweli ni maneno mazito sana au ni maneno ya nguvu sana kwa kiongozi. Hapo juu tunaona kuwa Paulo anamfundisha mwanawe wa kiroho Timoseo ili ajue umuhimu wa **kuvaa sura ya kiongozi**, au kuishi kwa kufuatana na **tabia za kiongozi**. Maneno mengine nitayafafanua huko mbele katika kitabu hiki, lakini la msingi kulishika katika andiko hilo ni **JIONYESHE KUWA UMEKUBALIWA NA MUNGU**. Paulo anafundisha hapo kuwa, uongozi au utumishi si kitu cha kuficha bali unatakiwa uonekane kwa watu wote. Aidha kiongozi anatakiwa kuanza yeye kujiamini kabla ya watu kumuamini.

## **CHUNGUZA ANDIKO HILI**

1 Timoseo 4:12.16 *Mtu awaye yote **asiudharau ujana wako**, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi. hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha. Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee. Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.*

Bwana asifiwe sana, ndugu msomaji, ninaposoma maandiko hayo huwa napata furaha sana na kuwa na nguvu nyingi sana. Paulo anamwambia Timoseo kuwa, **mtu asiudharau ujana wake**, ina maana Paulo anamuhimiza Timoseo kuidhirisha mamlaka yake ya kiongozi kwa watu ambao kwa kawaida wanajaribu kumdharau kwa sababu mbalimbali, lakini yeye asikubali mtu yoyote amdharau, hata kama hao watu wakifanya hivyo yeye aendelee kuwaonyesha kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu asiye kuwa na mashaka na utumishi wake.

Kujionyesha kuwa umekubalika ina maana kuwa hodari, kutokuogopa macho ya watu au mitazamo yao binafsi. Unajua unaweza kukutana na watu ambao wanaweza kukuvunja moyo kupitia mitazamo yao, ikiwa na maana unaweza kukutana na watu wanaokubeza. Kukuona wewe si lolote, lakini wewe waonyeshe kuwa wewe ni zaidi ya lolote. Katika kazi

ya Mungu mara nyingi tunakutana na upinzani, ijapokuwa tunafanya kazi ya kiroho na imani lakini usidanganyike ukadhani hautapata watu watakao kupinga ambao wamo ndani ya kanisa, lakini watakupinga na kutaka kukwamisha huduma yako, hivyo hauna budi kuwaonyesha watu kama hao kuwa wewe umekubalika na pia umeitwa na Mungu.